

ISTILAHIBUKA ZA TAALUMA ZA KISWAHILI VYUONI AFRIKA MASHARIKI

ISTILAHIBUKA ZA TAALUMA YA MAWASILIANO NA UANAHABARI KATIKA KISWAHILI VYUONI AFRIKA MASHARIKI

Stanley Adika Kevogo
surayangu@gmail.com

Ikisiri

Takribani taasisi zote za elimu ya juu katika eneo la Afrika Mashariki zimetokeleza mhamo wa ruwaza kutoka ufundishaji taaluma za Kiswahili kwa kutumia Kiingereza kwenda ufundishaji kwa kutumia Kiswahili chenyewe. Mazingira ya kuhawilisha maarifa kutoka lugha moja hadi nyingine aghalabu hulazimisha lugha lengwa kuunda istilahi kwa ajili ya kuyabeba maarifa hayo mapya. Hata hivyo, kuna upungufu wa istilahi za Kiswahili zinazohitajika kufanikisha mchakato huo. Kwa hali hiyo, jitihada zote zinapaswa kulengwa kwa utafiti, uundaji, usawazishaji na hatimaye usanifishaji wa istilahi. Makala hii inaangazia na kusambaza istilahi ibuka katika taaluma ya mawasiliano na uanahabari vyuoni Afrika Mashariki. Data itakayochambuliwa ni istilahi zilizotokana na mihadhara ya kozi za mawasiliano, uanahabari na mbinu za uhariri kwa Kiswahili. Istilahi zingine zimekusanywa kutoka kwa blogu na tovuti ya uanahabari zinazotumia Kiswahili. Pamoja na kubainisha ndaro wanazokabiliana nazo wanazuoni na wanahabari katika uendelezaji wake, uhakikiwa wa baadhi ya istilahi zinazotumika umefanywa ili kuthibitisha iwapo zinaakisi vyema maarifa yanayohusika na kwamba zinabeba dhana zilizokusudiwa kikamilifu.